

Waziri Kairuki avipa changamoto Vyombo vya Habari kubeba agenda ya Kampeni ya Kujenga na Kukuza Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa nchini.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Angellah J. Kairuki (Mb) amevitaka vyombo vya habari nchini kubeba agenda ya kampeni kuhusu Kujenga na Kukuza Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa nchini.

Mhe. Kairuki aliyasema hayo wakati akizindua Kampeni ya Kitaifa kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu, katika Ofisi za Takukuru jijini Dar es Salaam.

“Ninawaomba sana mtumie taaluma zenu na vyombo vyenu kuripoti na kuhamasisha wanajamii juu ya yale yatakayokuwa yanafanyika katika kipindi hiki cha kampeni pamoja na kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na kuzingatia misingi ya Uadilifu, Haki za Binadamu, Uwajibikaji na Utawala Bora katika maisha yao ya Kila siku” alisema Mhe. Kairuki.

Mhe. Kairuki aliongeza kusema kuwa Kampeni hiyo itaenda sambamba na utekelezaji wa shughuli mbalimbali ambazo ni pamoja na matembezi ya hiari kuhamasisha jamii juu ya Kauli Mbiu ya maadhimisho hayo, ambapo Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Mhandisi John W.H Kijazi atakuwa Mgeni Rasmi. Shughuli nyingine itakayofanyika katika maazimisho hayo ni Wiki maalum ya utoaji wa huduma kwa wananchi ambayo itazinduliwa katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia madhumuni ya Tanzania kuadhimisha siku ya Maadili na Haki za Binadamu, Mhe. Kairuki alibainisha kuwa ni kuliwezesha Taifa letu kutekeleza na kusimamia kwa vitendo dhana na misingi ya Maadili, Haki za Binadamu, Utawala Bora, Uwajibikaji na Mapambano dhidi ya Rushwa. Aidha, madhumuni mengine ni kuimarisha nidhamu katika Utumishi wa Umma na Taasisi za Sekta Binafsi ambazo zinafanya kazi na Serikali kwa ajili ya kuongeza kasi ya Maaendeleo kwa Taifa letu.

Pia, Mhe. Kairuki alieleza hadhara iliyohudhuria uzinduzi huo kuwa Serikali ya Awamu ya Tano, inayoongozwa na Mhe. Rais, Dkt. John Pombe Magufuli imedhamiria kwa dhati kupiga vita vitendo vya Rushwa, Uzembe, Ufisadi na Matumizi mabaya ya fedha za umma na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu kwa lengo la kuimarisha uzingatiwaji wa misingi ya Maadili, Uwajibikaji na Utawala Bora nchini. Hivyo, kampeni hii ya kuhamasisha uzingatiaji wa Maadili, Haki za Binadamu, Utawala Bora na kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa ni mojawapo ya juhudi za Serikali za kuwahamasisha na

kuwaelimisha wananchi kuikataa Rushwa, kuwa waadilifu na kutambua haki zao. Alisisitiza Mhe. Kairuki.

Akizungumzia umuhimu wa maazimisho hayo Mhe. Kairuki alisema kuwa itakuwa ni fursa kwa jamii kupata elimu kuhusu masuala ya Uadilifu, Haki za Binadamu, Uwajibikaji na Utawala Bora pamoja na kufahamu jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha mapambano dhidi ya Rushwa nchini.

“Serikali itajitahidi kuhakikisha kampeni hii inakuwa endelevu, ili kufikia azma ya kuwahudumia Wananchi wake kwa misingi ya Uwazi, Haki na Usawa bila kujali tofauti zao. Hivyo, natoa wito kwa wananchi na wadau wote kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa na ukiukwaji wa misingi ya Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji na Utawala Bora”. Alisisitiza Mhe. Kairuki.

Kwa mujibu wa Ratiba ya Kampeni hiyo, kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa kwa mwaka huu yatafungwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt John Pombe Magufuli tarehe 10 Desemba, 2016 katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.